# TAARIFA MUHIMU ZA KUWA NAZO MUOMBAJI WA HUDUMA ZA USAJILI WA NJE YA WAKATI (LATE REGISTRATION) WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR
# (Cheti cha kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka)

## KABLA HAJAANZA/KWENDA KUJAZA FOMU MTANDAONI
**CRVS - Online Application Check List**

Kabla muombaji hajaanza kujaza fomu ya maombi ya nje ya wakati (Late Registration) ya Usajili wa Matukio ya Kijamii (Cheti za Kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) Mtandaoni (Online Application) ni vizuri akawa na taarifa muhimu mkononi ili kuondoa usumbufu wa kutokamilisha taarifa au kujaza taarifa zisizo sahihi na uhakika:

https://ecrvs.zcsra.go.tz

## A. Usajili wa Nje ya Wakati wa Cheti za Kuzaliwa (Application for Late Registration of Birth).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **TAARIFA ZAKE ZA KUZALIWA (APPLICANT DETAILS):**
   Kwa anayeomba Cheti cha Kuzaliwa basi awe na taarifa anazojijuwa kuwa ni sahihi na uhakika za kuzaliwa kwake (Jina Lake, Tarehe ya kuzaliwa, pahali alipozaliwa/Mkoa/Wilaya / hospitali aliyozaliwa). Awe na sababu za kuchelewa kuomba cheti cha kuzaliwa pindi alipozaliwa na sababu ya kuomba cheti hicho kwa sasa.

2. **TAARIFA ZA BABA NA MAMA (PARENT DETAILS):**
   Awe na taarifa za Baba na Mama (Majina kamili, pahali walipozaliwa/hospital, Namba za Vitambulisho (ZanID-NIDA), Namba za cheti za kuzaliwa, pahali wanapoishi-makaazi, namba za nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia

3. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):**
   Awe au kuwe na taarifa za mtoa taarifa (Mdhamini) ikiwa anayefanya maombi si mwenyewe binafsi mfano mtoto lakini anayetoa taarifa za maombi ni baba, mama, Mjomba, Kaka nk. Taarifa hizo (Jina kamili, Namba ya Kiitambulisho (ZanID-NIDA), Namba ya cheti za kuzaliwa, pahali anapoishi-makaazi, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, **namba yake ya simu. Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarfia na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (kupokea control number kwa ajili ya kufanya malipo, kupokea kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya cheti husika. Na atapoenda Ofisi ya Wilaya basi ni lazima aende naye.

4. **TAARIFA ZA MAKAAZI:**
   Awe na taarifa za makaazi yake anapofanyia maombi yake (Pahali anapoishi, Shehia, namba ya nyumba, Mkoa, Wilaya n.k). Taarifa hizi zitathibitika kwa kuwa na barua ya Sheha inayothibitisha ukaazi wake.

5. **TAARIFA ZAKE BINAFSI ZA MAWASILIANO:**
   Awe na taarifa za mawasiliano yake binafsi (namba yake ya simu au barua pepe).

## B. Usajili wa Nje ya Wakati wa Cheti za Kifo (Application for Late Registration of Death).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **TAARIFA ZAKE ZA MAREHEMU (DECEASED DETAILS):**
   Kuwe na taarifa kamili binafsi za Marehemu, sababu/ugonjwa uliosababisha kifo, tarehe ya kifo, pahali kilipotokea kifo taarifa ziwe sahihi na uhakika (Namba ya Ktambulisho (ZanID-NIDA), Jina Kamili, Tarehe ya kuzaliwa, Umri, pahali kilipotokea kifo / hospital au nyumbani /Mkoa/Wilaya / Shehia). Kuwe na sababu za kuchelewa kuomba cheti cha kifo pindi kilipotokea na sababu ya kuomba cheti hicho kwa sasa. Awe na Nambari ya Kumbukumbu ya Cheti cha idhini ya Maziko na pahali alipozikwa marehemu.

2. **TAARIFA ZA MAKAAZI YA MAREHEMU:**
   Kuwe na taarifa za makaazi ya marehemu (Pahali alipokuwa anaishi, Shehia, namba ya nyumba, Mkoa, Wilaya, Jimbo n.k). Taarifa hizi zitathibitika kwa kuwa na barua ya Sheha inayothibitisha ukaazi wa marehemu.

3. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):**
   Kuwe na taarifa za mtoa taarifa za marehemu mfano baba, mama, Mtoto, Mjomba, Kaka nk. Taarifa hizi Jina kamili, Namba Kiitambulisho (ZanID-NIDA), Namba ya cheti za kuzaliwa, pahali anapoishi-makaazi, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, **namba yake ya simu. Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarifa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (kupokea control number kwa ajili ya kufanya malipo, kupokea kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya cheti husika

4. **TAARIFA ZA SHUHUDA WA KIFO (PERSON WHO WITNESS DEATH):**
   Kuwe na taarifa za aliyeshuhudia kifo cha marehemu ikiwa anayefanya maombi hakushuhudia kifo cha marehemu Taarifa hizo (Jina kamili, Namba ya Kiitambulisho (ZanID-NIDA), pahali pa kuzaliwa, pahali anapoishi-makaazi, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, namba yake ya simu.

## C. Usajili wa Nje ya Wakati wa Cheti za Ndoa (Application for Late Registration of Marriage).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **TAARIFA ZA NDOA (MARRIAGE INFORMATION):**
   Awe na taarifa za tukio la Ndoa (Pahali ndoa ilipofungwa Wilaya/Mkoa/Shehia, tarehe ilipofungwa ndoa, anayetoa taarifa hizo za ndoa Mke/Mume. Ndoa ya ngapi kwa wanandoa na kiwango cha mahali kilicholipwa na kama kuna kilichobaki. Awe na sababu za kuchelewa kuomba cheti cha Ndoa / sababu ya kuomba cheti hicho kwa sasa.

2. **TAARIFA ZA BWANA HARUSI (GROOM INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Bwana Harusi(Majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, pahali alipozaliwa Wilaya/Shehia/Jimbo, pahali anapoishi sasa/muda aloishi hapo, Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA) na Namba ya Simu ni muhimu sana.

3. **TAARIFA ZA BIBI HARUSI (BRIDE INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Bibi Harusi(Majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, pahali alipozaliwa Wilaya/Shehia/Jimbo, pahali anapoishi sasa/muda aloishi hapo, Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA), hali yake kabla ya kuolewa (Mwari, Mjane au yupo katika ndoa n.k) na Namba ya Simu ni muhimu sana.

4. **TAARIFA ZA SHAHIDI WA BWANA HARUSI (WITNESS INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Shahidi wa Bwana Harusi (Majina kamili, pahali anapoishi Wilaya/Shehia/Jimbo na Namba za Vitambulisho (ZanID-NIDA).

5. **TAARIFA ZA SHAHIDI WA BIBI HARUSI (WITNESS INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Shahidi ya Bibi Harusi (Majina kamili, pahali anapoishi Wilaya/Shehia/Jimbo na Namba za Vitambulisho (ZanID-NIDA).

6. **TAARIFA ZA MDHAMINI WA BIBI HARUSI (BRIDE GURDIAN INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Mdhamini wa Bibi Harusi (Majina kamili, pahali anapoishi sasa Wilaya/Shehia/Jimbo na Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA)

## D. Usajili wa Nje ya Wakati wa Talaka (Application for Late Registration of Divorce).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **TAARIFA ZA TALAKA (DIVORCE INFORMATION):**
   Awe na taarifa za tukio la Talaka (Pahali Takaka ilipotolewa Wilaya/Mkoa/Shehia, tarehe iliyotolewa Talaka, anayetoa taarifa hizo za Talaka Mke/Mume. Je ni Talaka ya ngapi kwa wanandoa hao (Kwanza, pili ua ya tatu). Awe na sababu za kuchelewa kuomba cheti cha Talaka na sababu ya kuomba cheti hicho kwa sasa.

2. **TAARIFA ZA MUME (GROOM INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Bwana Harusi(Majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, pahali alipozaliwa Wilaya/Shehia/Jimbo, pahali anapoishi sasa /muda aloishi hapo, Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA) na Namba ya Simu ni muhimu sana.

3. **TAARIFA ZA MKE (BRIDE INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Bibi Harusi(Majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, pahali alipozaliwa Wilaya/Shehia/Jimbo, pahali anapoishi sasa, muda aloishi hapo, Namba za Vitambulisho (ZanID-NIDA), hali yake ya ndoa kwa sasa na Namba ya Simu ni muhimu sana.

4. **TAARIFA ZA SHAHIDI WA MUME (WITNESS INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Shahidi wa Bwana Harusi(Majina kamili, pahali anapoishi sasa Wilaya/Shehia/Jimbo na Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA).

5. **TAARIFA ZA SHAHIDI WA MKE (WITNESS INFORMATION):**
   Awe na taarifa za Shahidi wa Bibi Harusi(Majina kamili, pahali anapoishi sasa Wilaya/Shehia/Jimbo na Namba za Vitambulisho(ZanID-NIDA).

## E. Maombi ya Kubadilisha Taarifa za Cheti za Kuzaliwa (Application for Updating Detail of Birth Certificate).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **KUWEPO KWA CHETI HUSIKA CHA KUZALIWA (CURRENT CERTFICATE):**
   Awe na Cheti cha kuzaliwa anachotaka kubadili taarifa kinachoonyesha (Nambari ya usajili wa cheti (Tukio), Majina kamili yaliyokuwa katika cheti. Awe na taarifa za kutaka mabadiliko kama ni jina kamili au herufi na sababu ya kuomba mabadiliko katika cheti hicho kwa sasa.

2. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):**
   Awe au kuwe na taarifa za mtoa taarifa ikiwa anayefanya maombi ya kubadilisha taarifa si mwenyewe binafsi mfano mtoto lakini anayetoa taarifa za maombi ya mabadiliko ni baba, mama, Mjomba, Kaka nk. Taarifa hizo (Majina kamili, Namba Kiitambulisho (ZanID-NIDA), pahali anapoishi-makaazi sasa, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, **namba yake ya simu. Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarifa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (control number kwa ajili ya malipo, kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya kubadili taarifa za cheti husika.

## F. Maombi ya Kubadilisha Taarifa za Cheti cha Kifo (Application for Updating Detail of Death Certificate).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **KUWEPO KWA CHETI HUSIKA CHA (CURRENT CERTFICATE):**
   Awe na Cheti cha kifo anachotaka kubadili taarifa kinachoonyesha (Nambari ya usajili wa cheti (Tukio), Majina kamili yaliyokuwa katika cheti. Awe na taarifa za kutaka mabadiliko kama ni jina kamili au herufi na sababu ya kuomba mabadiliko katika cheti hicho kwa sasa.

2. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):**
   Awe au kuwe na taarifa za mtoa taarifa anayefanya maombi ya kubadili taarifa. Taarifa hizo (Majina kamili, Namba Kiitambulisho (ZanID-NIDA), pahali anapoishi-makaazi, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, **namba yake ya simu. Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarifa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (control number kwa ajili ya malipo, kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya cheti husika.

## G. Maombi ya Kubadilisha Taarifa za Cheti cha Ndoa (Application for Updating Detail of Marriage Certificate).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **KUWEPO KWA CHETI HUSIKA CHA NDOA (CURRENT CERTFICATE):** Mume au Mke awe na Cheti cha Ndoa anachotaka kubadili taarifa kinanyoonyesha Nambari ya usajili wa cheti hicho/Tukio, Majina kamili yaliyokuwa katika cheti, kutaja mabadiliko kama ni ya jina kamili au herufi na sababu ya kuomba mabadiliko katika cheti hicho kwa sasa

2. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):** Mume au Mke awe au kuwe na taarifa za mtoa taarifa anayefanya maombi ya kubadili taarifa katika cheti cha ndoa. Taarifa hizo (Majina kamili, Namba Kiitambulisho (ZanID-NIDA), pahali anapoishi-makaazi sasa, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya na shehia, **namba yake ya simu. Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarifa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (control number kwa ajili ya malipo, kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya cheti husika.

## H. Maombi ya Kubadilisha Taarifa za Cheti cha Talaka (Application for Updating Detail of Divorce Certificate).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **KUWEPO KWA CHETI HUSIKA CHA TALAKA (CURRENT CERTFICATE):**
   Mume au Mke awe na Cheti cha Talaka anachotaka kubadili taarifa kinachoonyesha Nambari ya usajili wa Talaka/Tukio, Majina kamili yaliyokuwa katika Talaka, kutaja mabadiliko kama ni ya jina kamili / herufi na sababu ya kuomba mabadiliko katika cheti hicho cha talaka.

2. **TAARIFA ZA MTOA TAARIFA (INFORMANT DETAILS):**
   Mume au Mke awe au kuwe na taarifa za mtoa taarifa anayefanya maombi ya kubadili taarifa katika cheti cha talaka. Taarifa hizo (Majina kamili, Namba Kiitambulisho (ZanID-NIDA), pahali anapoishi-makaazi sasa, namba ya nyumba / Mkoa, Wilaya, shehia na namba yake ya simu. Namba ya Simu ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya mtoa taarifa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (control number kwa ajili ya malipo, kumbukumbu number (reference no) ya maombi ya Talaka husika.

## I. Maombi ya Kukata Rufaa (Application for Appeal).

Muombaji awe na taarifa zifuatazo:-

1. **TAARIFA ZA OMBI LA RUFAA (APPEAL INFORMATION):**
   Mtaka Rufaa awe na taarifa kamili za anachokatia rufaa (Cheti cha kuzaliwa, kifo, ndoa au talaka). Awe na Nambari ya kumbukumbu (Reference Number) ambayo atakuwa ametumiwa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar. Pia awe na sababu ya kukata rufaa na namba yake ya simu**.** **Namba ya Simu** ni muhimu kwani ndio itakayotumika kwa mawasiliano baina ya Mkata rufaa na Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

# CRVS Online Application forms

1. **UJAZAJI WA FOMU ZA MAOMBI YALIO NJE YA WAKATI (Yaliochelewa / Late Application) YA MATUKIO YA KIJAMII (kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) KWA NJIA YA MTANDAONI (ON-LINE APPLICATION)**

2. **UZAJAZI WA FOMU ZA MAOMBI YA KUFANYA MAREKEBISHO/KUSAHIHISHA TAARIFA KATIKA VYETI VYA (Kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) KWA NJIA YA MTANDAONI (ON-LINE APPLICATION)**

3. **UZAJAZI WA FOMU ZA MAOMBI YA KUKATA RUFAA BAADA KUKATALIWA OMBI HUSIKA (Kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) KWA NJIA YA MTANDAONI (ON-LINE APPLICATION)**

Nenda: https//ecrvs.zcsra.go.tz

**Kisha Fuata maelekezo**

# **T A N G A Z O**

**KUANZIA MWEZI WA MAY 2023**

1. **MAOMBI YOTE YALIYO NJE YA WAKATI (Late Application) YA MATUKIO YA KIJAMII (kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) YATAANZIA KWA KUJAZA FOMU MTANDAONI NA KUICHAPISHA (KU-PRINT) KISHA KUJA NAYO KATIKA AFISI ZA WILAYA ZA WAKALA KWA HATUA YA KUFANYIWA KAZI.**

2. **MAOMBI YOTE YA KUREKEBISHA/KUSAHIHISHA TAARIFA ZA VYETI VYA (kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) YATAANZIA KWA KUJAZA FOMU MTANDAONI NA KUICHAPISHA (KU-PRINT) KISHA KUJA NAYO KATIKA AFISI ZA WILAYA ZA WAKALA KWA HATUA YA KUFANYIWA KAZI.**

3. **MAOMBI YA KUKATA RUFAA BAADA KUKATALIWA OMBI LA TUKIO LA KIJAMII (Kuzaliwa, Kifo, Ndoa na Talaka) NAYO YATAANZIA MTANDAONI.**

**CRVS Online Application forms**

Nenda https://ecrvs.zcsra.go.tz Kisha Fuata maelekezo

A H S A N T E